Joseph Makoye

# Ninakuabudu Mungu Wangu




2. Mafahamu yangu yadanganya
Yanapokuona na kugusa
Namsadiki Yesu hadanganyi
Yeye Mungu Mwana na ukweli

3. Waficha Umungu msalabani
Na ubinadamu altareni
Nami na ungama yote mbili
Kama mwivi yule mwenye toba.

4. Thomaso aligusa majeraha
Nami nasadiki bila shaka
Ewe Yesu nipe pendo lako
Tumani kwako na imani

5. Umeteswa nini Bwana mwema
Kwa kunipa mkate wa uzima
Yesu unifiche ndani yako
Ili nilionje pendo lako

6. Yesu Pellicane utazame
Na kwa damu yako nitakase
Tone moja ndilo linatosha
na dunia yote yaokoka

7. Ndani ya mafumbo Yesu yumo
Utafunguliwa kwangu lini?
Nikuone Yesu uso wako
Nishiriki nawe heri yako Amina, Amina